# SHERIA YA WATU WENYE ULEMAVU 2010

# INATUAMBIA NINI?

## TAFSIRI RAHISI KWA USOMAJI WA WANANCHI






SWEDISH ORGANISATIONS OF PERSONS WITH DISABILITIES INTERNATIONAL DEVELOPMENT COORPORATION ASSOCIATION

**SHIA - OFISI YA TANZANIA**

MWANANYAMALA - KOMAKOMA

KITALU NA /30D

S L P 31676

DAR ES SALAAM, TANZANIA

Tunadai Jamii Shirikishi

We Demand For An Inclusive Society

Shirikisho la Vyama vya Watu wenye Ulemavu Tanzania (SHIVYAWATA)

MWANANYAMALA - VIJANA

KITALU NA. 367

S.L.P. 42984,

DAR ES SALAAM - TANZANIA

Tovuti: www.shivyawata.org



Kimechapishwa na: KAPERE PRINTING AND STATIONERY Mob: +255 655 / 755 352 214, +255 715 754 227 460

# SHERIA YA WATU WENYE ULEMAVU 2010

## INATUAMBIA NINI?

### TAFSIRI RAHISI KWA USOMAJI WA WANANCHI

**SHIA TANZANIA**

**Aprili, 2012**

**IMETOLEWA NA**

OFISI YA SHIA TANZANIA
KWA KUSHIRIKIANA NA SHIRIKISHO LA VYAMA VYA
WATU WENYE ULEMAVU TANZANIA
**(SHIVYAWATA)**

# SHERIA YA WATU WENYE ULEMAVU 2010

TAFSIRI RAHISI KWA USOMAJI WA WANANCHI

**Imeandaliwa na**
**Mtemi Gervas Zombwe,**

**Michoro:** Rashid Kagusa
**Tafsiri:** Wanasheria: Joseph Maganga na Robert Sizya
**Usanifu:** Shaaban Kimokole, Rashid Kagusa na Mtemi Zombwe

Unaruhusiwa kunakili sehemu yoyote ya kitabu hiki kwa minajili isiyo ya kibiashara. Unachotakiwa kufanya ni kunukuu chanzo cha sehemu iliyonakiliwa na kutuma nakala mbili SHIVYAWATA

# YALIYOMO

**SEHEMU YA I**
UTANGULIZI, MAANA NA MATUMIZI YA MANENO YALIYOTUMIKA .................................... 1

**SEHEMU YA II**
MISINGI NA WAJIBU WA KUTAMBUA HAKI ZA WATU WENYE ULEMAVU ............................ 4

**SEHEMU YA III**
UTARATIBU WA KITAASISI ........................................................................................... 7

**SEHEMU YA IV**
KUJUMUISHWA KWA WATU WENYE ULEMAVU .................................................................. 8

**SEHEMU YA V**
HUDUMA YA MISAADA KWA WATU WENYE ULEMAVU
KUTOKA MAMLAKA YA SERIKALI ZA MITAA ........................................................................ 10

**SEHEMU YA VI**
USAJILI WA WATU WENYE ULEMAVU NA MAKAZI .............................................................. 12

**SEHEMU YA VII**
HUDUMA ZA AFYA, ELIMU, UTENGEMAO NA AJIRA .......................................................... 13

**SEHEMU YA VIII**
KUFIKIKA KWA MAJENGO NA MAZINGIRA ASILI NA
UPATIKANAJI WA HUDUMA NA TAARIFA ............................................................................ 19

**SEHEMU YA IX**
USHIRIKI WA WATU WENYE ULEMAVU KATIKA
SHUGHULI ZA KISIASA NA KIJAMII ...................................................................................... 23

**SEHEMU YA X**
UTOAJI HUDUMA ZINAZOHUSIANA NA VIPINDI VYA LUNINGA
NA HUDUMA ZA SIMU ............................................................................................... 27

**SEHEMU XI:**
FEDHA KWA AJILI YA MFUKO ......................................................................................... 27

**SEHEMU YA XII**
MASHARTI MENGINEYO ................................................................................................. 28

**HITIMISHO** ............................................................................................................... 29

# SEHEMU YA I

# UTANGULIZI, MAANA NA MATUMIZI YA MANENO YALIYOTUMIKA

## UTANGULIZI

Hii ni "sheria ya watu wenye ulemavu ya mwaka 2010" ilipitishwa na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania mwezi Aprili mwaka 2010 na kusainiwa na Rais wa Tanzania tarehe 20 Mei 2010.

Sheria hii inatoa mwongozo wa kisheria wa namna ya kutoa huduma za afya, misaada ya kijamii, kufikika na kupitika kwa huduma na mazingira ya kijamii, huduma za utengemao, elimu na mafunzo ya ufundi, mawasiliano, ajira au hifadhi ya kazi na kudumisha haki za msingi za watu wenye ulemavu.

## MAANA YA MANENO MUHIMU YALITOTUMIKA

**"Ulemavu"** kukosa au kushindwa kuwa na fursa ya kushiriki katika maisha ya kawaida ya kijamii kwa kiwango sawa na wengine kwa sababu za kimaumbile, kiakili au sababu za kijamii.

**"Mtu mwenye ulemavu"** ni mtu mwenye udhaifu au upungufu wa viungo, fahamu au akili na ambaye uwezo wake wa utendaji kazi umepungua kutokana na vikwazo vya kimtazamo, kimazingira na kitaasisi.

**"Kufikika/Upatikanaji"** kuwezesha au kuruhusu mtu mwenye ulemavu kupata na kunufaika moja kwa moja au kwa njia nyingine huduma za kijamii za umma.

**"Afisa mwenye mamlaka"** ni afisa yeyote aliteuliwa na Kamishna kwa maandishi, kwa taratibu za kawaida au kimaalum kufanya kazi katika maeneo aliyopewa

**"Waziri"** Waziri mwenye dhamana ya kushughulikia watu wenye ulemavu

**“Mawasiliano”** ni pamoja na ya kuongea, lugha za alama, kuonesha ujumbe, breli, mawasiliano kwa ishara, maandishi makubwa, kupitia vyombo vya habari na pia sauti, michoro na teknolojia saidizi.

**“Ubaguzi”** ni kuzuiliwa au kutengwa kwa mtu kwa misingi ya ulemavu ambako kunafanyika kwa malengo, kuna madhara au kunalemaza na kumzuia mtu mwenye ulemavu kutambuliwa na kufurahia haki zake za binadamu katika nyanja za kisiasa, kijamii, kiuchumi na kiraia.

**“Ubaguzi chanya”** maana yake ni sera na taratibu zinazompendelea mtu mwenye ulemavu

**“Jengo la umma”** maana yake ni jengo au sehemu ya jengo, ambalo wanajamii au umma kwa ujumla wanafika na linamilikiwa, kutunzwa na kudhibitiwa na serikali au mtu binafsi anayetoa huduma kwa umma

**“Utengemao”** ni jitihada za pamoja za kuweka mazingira ya kufanikisha haki za watu wenye ulemavu katika nyanja zote za kijamii kama vile za afya, elimu, mafunzo ya ufundi, saikolojia, ikihusisha pia marekebisho ndani ya jamii na kukuza uelewa kwa umma ili kuinua kiwango cha utendaji wa mtu mwenye ulemavu na kumwezesha kuishi maisha ya kawaida.

**“Ulinzi wa kijamii”** ni mifumo ya usaidizi ya kifamilia au kijamii na michango ya nchi au wadau nje ya serikali inayowasaidia watu wenye ulemavu.

## MALENGO YA SHERIA HII

Kuweka mwongozo wa kisheria wa namna ya utekelezaji na utoaji huduma kwa watu wenye ulemavu katika mazingira jumuishi bila ubaguzi katika sekta na nyanja zote za kijamii.

Kujenga uelewa wa pamoja miongoni mwa wanajamii juu ya haki za watu wenye ulemavu na namna bora ya kuchangamana na kushirikiana katika mazingira mbalimbali ya kazi, kijamii na fursa za kiuchumi.

Kukuza uelewa miongoni mwa wana jamii juu wajibu na majukumu ya kila mwananchi na mamlaka mbalimbali za kijamii

kuhakikisha haki na fursa za watu wenye ulemavu zinaimarishwa ili kuondoa ubaguzi na kukondoisha masuala ya watu wenye ulemavu kwenye mifumo ya kijamii na kitaasisi ili kujenga jamii jumuishi inayowakubali watu wa aina zote.

## UMUHIMU WA KUWEPO KWA SHERIA HII

Inajenga mfumo wa kisheria na utaratibu wa utoaji na upatikanaji wa huduma kwa watu wenye ulemavu

Inaweka uhalali wa adhabu kwa watu wanaovunja haki za watu wenye ulemavu kwa maksudi au kwa kutojua

## SHERIA HII INA MUHUSU NANI?

Sheria hii inamhusu kila mtu aishiye Tanzania, kuanzia Mamlaka za kijamii, taasisi za kiserikali na zisizo za kiserikali.

## NANI MWENYE JUKUMU LA KUITEKELEZA?

Kila mtu aishiye Tanzania, taasisi, asasi au shirika lolote linalofanya kazi nchini Tanzania vina wajibu wa kuitekeleza sheria hii.

# SEHEMU YA II

# MISINGI NA WAJIBU WA KUTAMBUA HAKI ZA WATU WENYE ULEMAVU

## Kanuni muhimu za sheria (ibara 4)

- Kuheshimu utu wa mtu, uhuru wa kuchagua na kujitegemea kwa watu wenye ulemavu.
- Haki ya kushiriki na kushirikishwa kikamilifu kwa watu wenye ulemavu katika mambo yote ya kijamii.
- Hakuna ubaguzi wa aina yeyote kwa watu wenye ulemavu katika nyanja zote.
- Watu wenye ulemavu wajumuishwe kikamilifu katika nyanja zote za maisha.
- Fursa sawa kwa watu wenye ulemavu.
- Kuwepo na usawa kati ya wanawake na wanaume wenye ulemavu na kutambuliwa kwa haki na mahitaji yao.




## Wajibu muhimu wa kutambua haki za watu wenye Ulemavu (ibara ya 5):

**Waziri husika atapaswa kufanya yafuatayo"**

- atasimamia haki za watu wenye ulemavu kama zilivyotajwa katika sheria hii;
- atachukua hatua madhubuti kulinda na kuleta uelewa wa haki za watu wenye ulemavu katika sera za taifa, mipango na utungaji wa sheria

Je, unafahamu kuwa kumcheka na kumdhihaki mtu mwenye ulemavu ni kosa kisheria?

- ataepuka kujihusisha na jambo au kitu chochote ambacho hakiendani na Sheria hii, na kuhakikisha kwamba mamlaka



zote za serikali na taasisi wanatenda kuendana na sheria hii.

- kwa kushirikiana na asasi za kiraia na wadau wengine atatakiwa kuchukua hatua muafaka ili kukuza uelewa katika jamii yote kuhusu viwekezo, mchango na haki za watu wenye ulemavu na kukuza utu na haki zao kupambana na upotoshaji, chuki na vitendo viovu dhidi ya watu wenye ulemavu katika nyanja zote za maisha.

## Usawa na kukomesha ubaguzi (ibara ya 6)

- Serikali itahakikisha kuwa watu wote wenye ulemavu ni sawa, na wanatambulika pasipo ubaguzi wa aina yoyote kulinda na kunufaika na yote yaliyomo katika Sheria hii;
- Serikali itazuia ubaguzi wa aina yoyote unaofanywa kwa misingi ya ulemavu na kuwahakikishia haki sawa watu wenye ulemavu na ulinzi madhubuti wa kisheria dhidi ya ubaguzi aina zote; na kwa lengo la kukuza usawa na kuondoa ubaguzi wa aina zote.
- Serikali itachukua hatua muafaka kuhakikisha mabadiliko ya msingi yanafanywa kuwasaidia watu wenye ulemavu wa rika na jinsia zote.

# SEHEMU YA III

# UTARATIBU WA KITAASISI

## Kuundwa kwa Baraza la Ushauri la Taifa (ibara ya 8)

- Kutakuwa na Baraza lijulikanalo kama Baraza la Ushauri la Taifa kwa ajili ya Watu wenye Ulemavu.
- Wajumbe wote wa baraza isipokuwa Mwenyekiti watateuliwa na Waziri.
- Kamishna ndiye atakuwa Afisa msimamizi wa shughuli za kila siku za Baraza na mkuu wa Sekretarieti.

## Wajibu na Mamlaka ya Kamishna (ibara ya 9)

- Kutunza taarifa na takwimu za watu wenye ulemavu.
- Kurekodi na kutunza taarifa za makazi ya watu wenye ulemavu.
- Kutoa leseni, kusimamia au kufuta usajili wa makazi ya watu wenye ulemavu.
- Kusimamia kazi za maafisa wenye mamlaka.
- Kusimamia fedha zinazotolewa na baraza.
- Kuagiza, kudai na kupokea ripoti za robo mwaka kutoka katika taasisi za watu wenye ulemavu, na kwa ajili ya watu wenye ulemavu.
- Kukagua zana za kutolea huduma kwa watu wenye ulemavu kufuatana na taratibu za sheria hii.
- Kuingia katika eneo lolote ili kuchunguza utekelezaji wa taratibu za sheria hii.

## Kazi za Baraza (ibara ya 12)

- Kumshauri waziri kuhusu huduma za watu wenye ulemavu.
- Kutoa ushauri katika mashirika na taasisi zinazoandaa huduma na program kwa watu wenye ulemavu.
- Kutoa ushauri kuhusu hatua zinazoweza kuchukuliwa kuhusu ubaguzi wa watu wenye ulemavu.
- Kuishauri tume ya uchaguzi juu ya watu wenye ulemavu na ushiriki wao kikamilifu kwenye chaguzi mbalimbali.
- Kushauri kuhusu uwepo wa uhifadhi wa kumbukumbu sahihi za watu wenye ulemavu na taasisi zao.
- Kuhakikisha hali ya mikataba ya kazi katika sekta binafsi na za umma inakuwa ya uhakika kwa watu wenye ulemavu.

# SEHEMU YA IV

# KUJUMUISHWA KWA WATU WENYE ULEMAVU

## Kuishi kwa kujitegemea na kushirikishwa katika jamii (ibara ya 15)

- Kila mtu mwenye ulemavu atasaidiwa na mamlaka ya serikali yake ya mitaa, ndugu, mashirika ya walemavu, mashirika ya umma au mtu yeyote kadri inavyowezekana kuishi kwa kujitegemea na kujumuishwa katika jamii.
- Mtu mwenye ulemavu hatalazimishwa kuishi katika taasisi au kwenye mfumo fulani wa maisha kijamii ikiwemo katika makazi ya walemavu.
- Waziri kwa kushirikiana na Baraza, atapanga taratibu na kuchukua hatua madhubuti ikiwa itahitajika kufanya hivyo ili kusaidia na kuwawezesha watu wenye ulemavu kujitegemea na kujumuika kikamilifu katika jamii, ikiwemo kutoa fursa sawa kwa mtu mwenye ulemavu kuchagua eneo la kuishi na mfumo wa kuishi kulingana na sheria nyingine.

## Wajibu wa kutoa msaada wa kijamii kwa watu wenye ulemavu (ibara ya 16)

- Ndugu wote wa mtu wenye ulemavu wana wajibu wa pamoja wa kumpatia msaada wa kijamii mtu huyo.

## Kushindwa kutoa msaada stahiki (ibara ya 17)

- Inapothibitika kwamba ndugu amezembea kutoa msaada unaokidhi kijamii kwa mtu mwenye ulemavu mahakama inaweza, kwa kufuatia

> Je, unafahamu kuwa kushindwa au kuzembea kutoa msaada kwa ndugu mwenye ulemavu ni kosa kisheria?

maombi ya aidha mlemavu mwenyewe au wakili, kuamuru ndugu huyo kulipa kiasi hicho cha pesa kila mwezi kama itakavyoonekana inafaa.

- Mahakama inaweza, kila baada ya kipindi fulani kubadili au kufuta agizo lolote la awali lililoagizwa kwa mtu aliyeshindwa kutoa msaada kwa ndugu mwenye ulemavu.



## SEHEMU YA V

# HUDUMA YA MISAADA KWA WATU WENYE ULEMAVU KUTOKA MAMLAKA YA SERIKALI ZA MITAA


### Wajibu wa mamlaka ya serikali za mitaa kuwalinda watu wenye Ulemavu (Ibara ya 20)

- Kulinda na kudumisha haki na ustawi wa mtu mwenye ulemavu ndani ya eneo la utawala wake.

- Kupitia kwa Afisa Ustawi wa Jamii itatoa ushauri kwa wazazi, walezi, ndugu na watu wenye ulemavu ili kuondoa au kupunguza unyanyapaa na ubaguzi.

- Kutoa msaada/kuwezesha watu wenye ulemavu ili waweze kuendeleza vipawa na uwezo walio nao kwa ajili ya kujitegemea.

- Kuandaa na kutunza rejesta ya usajiri wa watu wenye ulemavu na kuwasilisha maelezo hayo kwa kamishna wa Ustawi wa Jamii


MHESHIMIWA SPIKA
VIFAA VYA WATU WENYE ULEMAVU
NI GHARI SANA KUANZIA MAFUTA
KWA AJILI YA ALBINO, BRAILE
ZA KUANDIKIA, SHIME SIKIO,
NA HATA FIMBO NA BAISKELI
ZA KUTEMBELEA,
WALEMAVU WA VIUNGO
VINA BEI KUBWA SANA,
SERIKALI HAIWEZI
SI KWELI WAZIRI
HAKUNA KIFAA HATA KIMOJA
KINACHOGHARIMU FEDHA NYINGI
KAMA GARI UNALOTEMBELEA,
KAMA HELA ZA SHANGINGI LAKO
ZILIPATIKANA BASI NA ZA VIFAA
ZINAWEZA KUPATIKANA
NI UTASHI TUU....!
MBUNGE
MBUNGE
MBUNGE
WAZIRI
WAZIRI
WAZIRI

# SEHEMU YA VI

# USAJILI WA WATU WENYE ULEMAVU NA MAKAZI

## Rejesta ya watu wenye ulemavu (ibara ya 23)

- Kamishna baada ya kushauriana na Baraza, ataweka na kutunza rejesta ya watu wenye ulemavu na makazi yao itakayojulikana kama rejesta ya Watu wenye Ulemavu.
- Watu wote wenye ulemavu na makazi yao wataandikishwa kwenye daftari maalumu litakalojulikana kama Rejesta ya Watu wenye Ulemavu.
- Rejesta hiyo itatumika tu kwa ajili ya utambulisho wa watu wenye ulemavu na malengo mengine ya takwimu;
- Pia itatoa utaratibu kwa kutuma maombi ya hitaji la kuanzisha, kuendesha na kusimamia makazi kwa watu wenye ulemavu.

> Je, unafahamu kuwa watu wote wenye ulemavu wanapaswa kusajiriwa kwenye rejesta maalumu ili kutambuliwa kiurahisi?

## Kujiondoa katika rejesta na masharti ya makazi ya watu wenye ulemavu (ibara ya 24&25)


- Hakuna mtu mwenye ulemavu atakayeondoa jina lake katika rejesta wakati akingali na ulemavu.
- Mtu haruhusiwi kuanzisha, kuendesha, kuongoza au kuratibu makazi ya watu wenye ulemavu isipokuwa makazi hayo yawe yamesajiriwa.
- Mtu anayetaka kuanzisha, kuendesha, kuongoza au kuratibu makazi yawatu wenye ulemavu atatuma maombi kwa Kamishna ili kusajili makazi hayo. Kamishna anaweza kuagiza ukaguzi ufanywe katika eneo hilo linalotaka kutumika kwa makazi ya watu wenye ulemavu.

# SEHEMU YA VII

# HUDUMA ZA AFYA, ELIMU, UTENGEMAO NA AJIRA

## Huduma bora za afya na utengemao (ibara ya 26)

- Waziri atahakikisha mfumo wa maadili ya huduma binafsi na huduma za umma zinakuwa bora, zinatolewa kwa uwazi na kuheshimu utu na uhuru wa kuamua kwa watu wenye ulemavu
- Kila kituo cha kutoa huduma za afya kiwe binafsi au cha umma hakitamnyima mtu mwenye ulemavu haki ya kupata huduma za afya na kitatakiwa kuchukua hatua madhubuti kuhakikisha mtu huyo anapata huduma za afya.



- Mtu mwenye ulemavu atastahili kupokea taarifa sahihi zinazohusiana na afya kwa mfumo au njia inayoweza kumfikia.
- Waziri baada ya kushauriana na Baraza, atahakikisha kwamba-mfumo wa maadili ya huduma binafsi na huduma za umma, zinakuza huduma bora, uwazi na kuheshimu haki, utu na uhuru wa kuamua kwa watu wenye ulemavu. Na wataalamu wa huduma za afya wanatoa taarifa kwa watu wenye ulemavu na kutenda haki.


Je, unafahamu kuwa kujenga majengo yasiyo rafiki kwa watu wenye ulemavu ni ubaguzi na ni kosa kisheria?

- Itakuwa ni kosa kwa mujibu wa Sheria hii kumkatalia au kumbagua mtu mwenye ulemavu ili asipate huduma za afya na uwezeshwaji.

## Elimu na mafunzo kwa watu wenye ulemavu (ibara ya 27)

- Watu wenye ulemavu, wa umri na jinsia yoyote watakuwa na haki sawa ya kupata elimu, mafunzo mazingira shirikishi na manufaa ya tafiti kama raia wengine.
- Kila mtoto mwenye ulemavu atakuwa na haki sawa ya kuandikishwa katika shule binafsi au za umma.
- Kila mtoto mwenye ulemavu atasoma katika shule za umma au binafsi za kawaida isipokuwa pale itakapoonekana ana mahitaji maalumu.
- Mtoto anayetajwa katika kipengele kidogo cha (3) atapatiwa msaada maalumu unaoendana na ulemavu wake au huduma maalumu za kujifunzia kutoka kwa mwalimu mwenye sifa stahiki aumwalimu aliyekabidhiwa jukumu hilo.
- Shule maalum zitakuwa za mpito kuelekea shule jumuishi.

Je, unafahamu kuwa watu wenye ulemavu watasoma kwenye shule za kawaida?




## Kuzuia ubaguzi katika taasisi za elimu (ibara ya 28)

Kila taasisi ya elimu itakuwa na jukumu la kutoa elimu kwa wote bila kuwabagua watu wenye ulemavu. Itahesabika ni ubaguzi pale ambapo taasisi:-

- itashindwa au itakataa kumsajili/kumwandikisha mtu kwa kigezo cha ulemavu
- itamnyima au itamwekea mipaka mtu mwenye ulemavu kufikia au kupata huduma au manufaa yanayotolewa na taasisi hiyo ya elimu;
- kumfukuza mtu mwenye ulemavu kwa sababu zinazohusiana na ulemavu wake;
- Ikijenga shule na miundombinu ambayo ni vigumu kutumia kwa watu wenye ulemavu.

Je, unafahamu kuwa kila mwajiri anatakiwa kutenga nafasi za ajira kwa watu wenye ulemavu kwa 3%?




## Vifaa/Nyenzo kwa ajili ya watu wenye ulemavu (ibara ya 29)

- Kila meneja au mmiliki wa taasisi ya elimu atatakiwa kuzingatia mahitaji maalumu ya watu wenye ulemavu
- Mtu yeyote anayemiliki au kuendesha shule maalumu ya watu wenye ulemavu atatakiwa kutoa vifaa vya kutosha kwa ajili yao.

## Wajibu wa kutoa ajira na kuendelea ajira kwa watu wenye ulemavu (ibara ya 31 na 32)

- Kila mwajiri wa umma au binafsi, panapokuwa na nafasi yakazi inayofaa kwa mtu mwenye ulemavu na ameiomba nafasi hiyo, awape watu wenye ulemavu ambao wamefikia kiwango cha sifa zinazotakiwa kwa ajira hiyo.
- Waziri kwa kushauriana na Waziri wa kazi, wataandaa kanuni zinazomtaka kila mwajiri mwenye wafanyakazi kuanzia ishirini

na kuendelea kuajiri watu wenye ulemavu kwa mfumo kutenga idadi ya upendeleo na kuhakikisha asilimia tatu ya waajiriwa ni watu walemavu.

- Kila mwajiri atawasilisha ripoti ya mwaka kwa Kamishna kuhusu taarifa ya ajira ya watu wenye ulemavu walioajiriwa ofisini kwake, katika eneo lake la kazi, taasisi au shirika.
- Kwa lengo la kurejesha na kulinda ajira za watu wenye ulemavu kila mwajiri atatakiwa kuweka juhudi kuendelea kuajiri watu wenye ulemavu katika eneo lake la kazi.

## Kukataza na kuzuia ubaguzi katika ajira kwa watu wenye ulemavu (ibara ya 33)

Mwajiri hatamtendea mtu mwenye ulemavu tofauti na asiye na ulemavu kuhusiana na:-


- tangazo la ajira;uandikishaji watu katika ajira
- kutoa vigezo au masharti ya ajira
- kuandaa, kupanga makundi au kufuta kazi au nafasi ya kazi;
- uamuzi au ugawaji ujira, mishahara, likizo au makazi, na posho nyinginezo
- mafunzo, kuendelezwa, muda wa kujifunza (uanagenzi), kuhamishwa, kupandishwa cheo au kupunguzwa kazi
- ugawaji wa vifaa vinavyohusiana ajira au vya kazi na
- ugawaji wa mapato mengine ya ziada au masuala mengine yanayohusiana na kazi.

## Mazingira ya kazi kwa watu wenye ulemavu (ibara ya 34)

Ili kuweka mazingira ya kazi kuwa rafiki kwa watu wenye ulemavu waajiri watatakiwa kufanya yafuatayo;

- Kuchukua hatua kadri iwezekanvyo kuboresha mazingira ya kazi ili kuzuia kuumia, kujeruhiwa au kupata ulemavu.
- Kuhakikisha kuna mazingira salama kikazi na kiafya kwa watu wenye ulemavu.
- Kuwalinda watu wenye ulemavu dhidi ya unyanyaswaji.
- Kuruhusu watu wenye ulemavu kufurahia haki zao za ajira na kujiunga na vyama vya wafanyakazi kwa mujibu wa sheria ya haki za watu wenye ulemavu.
- Kuwawezesha wafanyakazi wenye ulemavu kupata miongozo na maelekezo ya kitaalamu, kimafunzo na kuendelea na mafunzo kwa ajili ya kuendeleza taaluma zao.

- Waziri atahakikisha wafanyakazi wenye ulemavu wanabaki kazini na mfanyakazi yeyote aliyepata ulemavu akiwa kazini anaruhusiwa kurudi kazini.
- Kufanya marekebisho stahiki sehemu za kazi na kutoa vitendeakazi.




# SEHEMU YA VIII

# KUFIKIKA KWA MAJENGO NA MAZINGIRA ASILI NA UPATIKANAJI WA HUDUMA NA TAARIFA

## Kupitika na kufikika kwa majengo ya umma (ibara ya 35)

- Waziri kwa kushauriana na Waziri anayehusika na majengo na kwa kadri inavyowezakana, atahakikisha kwamba majengo ya umma na majengo mengine yanayotoa huduma kwa wananchi yanapitika na kufikika na watu wenye ulemavu
- Waziri kwa kushauriana na Baraza, ataandaa taratibu wa

Je, unafahamu kuwa kujenga jengo lenye ngazi bila kuwa na njia za watu wenye ulemavu ni kosa?



jinsi ya kufikika kwa majengo ya umma kwa lengo la kutoa mwongozo kwa vyombo binafsi na vya umma.

- Kila chombo cha umma au binafsi kitafuata taratibu hizo kwa kiwango kinachotakiwa na kadri iwezekanavyo, kitafanya hivyo wakati wa ujenzi, wakati wa kubadilisha vitu au kupanua jengo la umma.




## Kupata huduma zitolewazo na taasisi za umma (ibara ya 36)

- Huduma zote zinazotolewa na chombo/taasisi za umma na zinapaswa kuwafikia watu wote wakiwemo watu wenye ulemavu. Na mkuu wa taasisi hiyo anapaswa kuhakikisha hilo linafanyika
- Pale inapobidi itatakiwa kuwepo na mtu mwenye utaalamu na ujuzi stahiki kutoa ushauri kwa taasisi/chombo hicho juu

ya namna kuhakikisha huduma zinazotolewa na taasisi/ chombo hicho zinawafikia watu wenye ulemavu

- Katika kila shirika au taasisi kunapaswa awepo angalau mtu mmoja atakaye ratibu usaidizi na kuwaongoza watu wenye ulemavu kupata huduma zao

## Kufikika kwa maeneo ya kumbukumbu asili za kihistoria na utalii kwa watu wenye ulemavu

- Mkuu wa chombo cha umma, kwa kadri inavyowezekana, atahakikisha kwamba eneo lote au sehemu za kumbukumbu za kihistoria na vivutio au shughuli za utalii zilizopo katika jamii vinafikiwa na watu wenye ulemavu kwa mujibu wa Sheria hii.

## Kupata taarifa na kuondoa vizuizi vya kuyafikia maeneo (ibara ya 38, 48 na 50)


- Maudhui ya taarifa mbalimbali yanapaswa kuwasilishwa kwa namna na lugha ambayo inajulikana kwa watu wenye ulemavu.
- Kwa mawasiliano yanayofanywa kwa njia za kielektroniki teknolojia asilishi zinapaswa kuwepo ili kuhakikisha taarifa hiyo inawafikia watu wenye ulemavu, hasa wasioona

> Je, unafahamu kuwa ni kosa kumzuia mtu mwenye ulemavu kuingia sehemu yoyote ambamo watu wasio na ulemavu wameingia?

- Taarifa zinazowahusu watu wenye ulemavu wa akili zinapaswa kuwasiliswa kwa lugha nyepesi na wazi inayoeleweka kiurahisi kwao.
- Watu wote wenye ulemavu wana haki ya kuishi maeneo yasiyo na vizuizi kwao kupita au kupata huduma, na yenye mazingira rafiki kwao yanayo wawezesha kuyafikia majengo na miundo mbinu ya umma kama vile barabara, mawasiliano na huduma nyingine za kijamii zinazosaidia na kukuza ujongeaji wao.
- Wasanifu majengo, wahandisi wa ujenzi na watu wengine wanaohusika katika kubuni na kujenga majengo na

miundombinu ya umma wanatakiwa kufuata matakwa ya upitikaji na ufikikaji ili kuhakikisha kuwa majengo mapya, barabara, viwanja vya michezo, vifaa vya usafiri na ukarabati wa miundombinu ya zamani ifuate usanifu unaofikika na kupitika na watu wenye ulemavu.

- Ziandaliwe kanuni zitakazo agiza kuwekwa alama za barabarani na majengo kwa ajili ya utekelezaji wa mahitaji haya.
- Itakuwa ni kuvunja sheria kwa mtu mwenye ulemavu kwa sababu ya ulemavu wake, kunyimwa au kukataliwa ruhusa ya kuingia katika eneo lolote ambalo wanajamii wa kawaida wanaruhusiwa kuingia.




# SEHEMU YA IX

# USHIRIKI WA WATU WENYE ULEMAVU KATIKA SHUGHULI ZA KISIASA NA KIJAMII

## Ushiriki wa watu wenye ulemavu katika shughuli za kisiasa na kijamii (ibara ya 51)

Kila mtu mwenye ulemavu ambaye amefikisha umri wa miaka kumi na nane na kuendelea ataruhusiwa kufurahia na kutumia haki zake za kisiasa na fursa pasipo kubaguliwa sawa na raia mwingine yeyote.

Mtu mwenye ulemavu atakuwa na haki ya kupiga kura, kushika wadhifa katika jamii au kushiriki katika fursa na haki za kisiasa



sawa na raia wengine bila ubaguzi wa aina yoyote.

Waziri baada ya kushauriana na Baraza na Tume ya Taifa ya Uchaguzi atahakikisha;

- Haki na fursa ya watu wenye ulemavu ya kuchagua na kuchaguliwa inatekelezwa
- Utaratibu mzima wa kupiga kura unakuwa rafiki kwa watu wenye ulemavu, (vituo vinafikika na rafiki kwa watu wenye ulemavu. Na kuhakikisha vifaa na mahitaji yote ya wapiga kura kwa watu wenye ulemavu vinapatikana).
- watu wenye ulemavu wana uhuru wa kuchagua kama wapiga kura halali, na inapobidi kwa kuomba kwao wasaidiwe kupiga kura na watu watakaowachagua wao wenyewe.
- Anatoa mafunzo kwa wasimamizi wa wapiga kura kuhusu haki za watu wenye ulemavu
- Pale ambapo sehemu ya kupiga kura iliyotajwa kwenye sehemu hii si rafiki kwa watu wenye ulemavu eneo mbadala litatafutwa na kutangazwa kutumiwa na watu wenye ulemavu.

## Kushiriki katika Michezo, starehe na burudani (ibara ya 52)

Waziri baada ya kushaurina na Baraza na Waziri anayehusika na michezo utamaduni, atachukua hatua muafaka:-

- Kuchochea na kuhamasisha ushiriki wa watu wenye ulemavu katika shughuli za michezo katika ngazi zote.
- Kuhakikisha kwamba watu wenye ulemavu wanapata fursa ya kuandaa, kuendeleza na bila woga kushiriki katika michezo na burudani maalumu kwa watu wenye ulemavu.
- Kusisitiza wapewe maelekezo sahihi, mafunzo na zana kwa ajili ya shughuli zao za michezo na burudani.
- Kuwahamasisha watu wenye ulemavu kufika katika viwanja na maeneo ya michezo, burudani na utalii.
- Kuhakikisha kwamba watoto wenye ulemavu wanapata fursa sawa ya kushiriki kucheza, burudani, starehe na shughuli nyingine za michezo.



## Kushiriki katika maisha ya utamaduni (ibara ya 53)

- Mtu mwenye ulemavu atakuwa na haki ya kushiriki kama raia mwingine yeyote katika maisha ya kitamaduni katika jamii bilakubaguliwa.
- Serikali kwa kushirikiana na vyama vya kiraia, itachukua hatua muafaka kuwawezesha watu wenye ulemavu kupata fursa za kukuza na kuendeleza vipaji vyao vya kibunifu, kisanaa na kiakili kwa manufaa yao binafsi na kwa manufaa ya umma.
- Waziri kwa kushauriana na Baraza la Waziri anayeshughulikia utamaduni, atachukua hatua madhubuti kuhakikisha kwamba, watu wenye ulemavuwanafurahia kupata vifaa vyote vya kitamaduni kwa mifumo rafiki kwao, wanafurahia

kuona vipindi vya luninga, filamu, kumbi za maonesho, maeneo ya kihistoria n.k.

- Lugha ya alama, kugusa na kupapasa kwa viziwi wasioona (tactile), fimbo nyeupe na maandishi ya nukta nundu zitahamasishwa na kutambulika kama njia rasmi za mawasiliano.

## Ulinzi wa kijamii kwa watu wenye ulemavu (ibara ya 54)

- Mtu mwenye ulemavu atastahili kupewa ulinzi wa kijamii pasipo kubaguliwa kwa misingi ya ulemavu wake.
- Waziri baada ya kushauriana na Baraza na Waziri anayeshughulikia kazi, fedha na ajira, atachukua hatua madhubuti kuhakikisha watu wenye ulemavu wanafurahia kupata kinga na ulinzi wa kijamii, ikiwemo hatua ya-kuhakikisha wanapata vifaa, huduma sahihi na kwa gharama nafuu, na pia misaada ya mahitaji mengine yanayohusiana na ulemavu; na
- Kuhakikisha watu wenye ulemavu hasa wazee na wanawake, wanaingia katika mipango ya hifadhi ya jamii na mikakati ya kupunguza umasikini na wanapata ruzuku na mikopo kwa shughuli za kuzalisha kipato.

Je, unafahamu kuwa watu wenye ulemavu wana haki ya kupata mikopo kwa ajili ya kujiingizia kipato zaidi?

## SEHEMU YA X

## UTOAJI HUDUMA ZINAZOHUSIANA NA VIPINDI VYA LUNINGA NA HUDUMA ZA SIMU

### Program za Televisheni/Luninga na Huduma za Simu (ibara ya 55 na 56)

- Vituo vyote vya luninga vitawekwa wakalimani wa lugha za alama katika matangazo yote ya habari, vipindi vya elimu na vipindi vingine vinavyogusa matukio ya kitaifa.
- Watu wote wanaotoa huduma za simu kwa umma, wanatakiwa kufanya kila liwezekanalo kuweka vifaa maalumu vya simu au vitengo kwa ajili ya watu wenye matatizo ya kusikia na alama za kugusa kwenye simu kuwawezesha watu wenye ulemavu wa macho kuwasiliana kwa njia ya simu.

## SEHEMU XI

## FEDHA KWA AJILI YA MFUKO

### Sheria imeanzisha Mfuko utakaojulikana kama Mfuko wa Taifa wa watu wenye ulemavu utakaosimamiwa na Ofisi ya Kamishna

**Vyanzo vya fedha ya mfuko huu ni:**

- Fedha ikayopitishwa na Bunge kwa madhumuni ya mfuko huu
- Ada au kiasi cha fedha kinachoweza kulipwa katika Mfuko katika utekelezaji wa

Je, unajua kuwa kutakuwa na mfuko wenye fedha za kugharamia elimu ya watu wenye ulemavu?

majukumu yake chini ya Sheria hii

- Fedha yoyote halali itokanayo na Mfuko huu na
- Fedha nyingine yoyote halali itakayotolewa kwa ajili ya mfuko huu.

## Matumizi ya fedha za Mfuko wa watu wenye Ulemavu

- Kugharamia elimu na mafunzo ya ufundi stadi kwa watu wenye ulemavu
- Kugharamia program za utengemao wa kifedha kwenye masuala ya ulemavu na dharura
- Kutoa ruzuku kwa asasi za watu wenye ulemavu
- Kuchangia utafiti juu ya ulemavu na mambo mengine yanayohusiana na ulemavu
- Na kufanya jambo lolote muhimu katika kukuza na kuboresha malengo ya fedha za mfuko huu.

# SEHEMU YA XII

# MASHARTI MENGINEYO

## Mamlaka ya kuingia na kukagua pamoja na mgawanyo wa madaraka (ibara ya 59, 60 na 61)

- Kamishna au afisa yeyote aliyetumwa, kila wakati itakapohitajika, ataingia katika eneo lolote la mwajiri, taasisi, shirika au jengo kwa lengo la kukagua na kuhakikisha kama yanayofanywa yanaendana na Sheria hii.
- Kamishna kwa maandishi, anaweza kumteua mtu yeyote kuwa afisa ili kutekeleza Sheria hii.

Je, unafahamu kwamba kufanya kinyume na sheria ya watu wenye ulemavu ya 2010 ni kosa linalostahili adhabu?

- Kamishana anaweza kukasimisha madaraka kwa idara yeyote ya serikali au mtu yeyote kwenye idara kufanyakazi za sheria hii kutokana na malaka aliyopewa na sheria hii
- Waziri kwa kushauriana na Baraza anaweza kutunga kanuni zitakazotumika kwenye kusajiri, kupima viwango na kusimamia makazi ya watu wenye ulemavu.
- Taasisi yoyote au mtu binafsi atakayegundulika anafanya kinyume na sheria hii atakuwa amefanya kosa ambalo atastahili adhabu kwa mujibu wa sheria hii.

## HITIMISHO

Utekekelezaji wa sheria hii utahitaji kubadili mitazamo kwa kiwango kikubwa kuanzia kwa wananchi, viongozi, taasisi, mashirika na asasi mbalimbali ndani ya jamii. Kubadili fikra na mitazamo ndiyo hatua muhimu itakayopelekea kubadilisha matendo na fikra za wananchi juu ya watu wenye ulemavu. Pia itasaidia kufanikiwa kivitendo harakati za wadau wengi za kukondoisha masuala ya watu wenye ulemavu katika nyanja zote za maisha kiuchumi, kisiasa na kiutamaduni.

Kuwa na jamii jumuishi isiyo na ubaguzi ni jambo linalowezekana likianza na mtu mmoja mmoja, taasisi na jamii kwa ujumla.

Sheria hii inatoa mwongozo wa kisheria wa namna ya kutoa huduma za afya, misaada ya kijamii, kufikika na kupitika kwa huduma na mazingira ya kijamii, huduma za utengemao, elimu na mafunzo ya ufundi, mawasiliano, ajira au hifadhi ya kazi na kukuza haki za msingi za watu wenye ulemavu.

**Sheria hii ni mahali pa kuanzia kuelekea ushindi huo!**

## SHUKRANI

Kazi hii ni matokeo ya ushirikiano wenye mafanikio baina ya vyama vya watu wenye ulemavu Sweden chini ya shirikisho la **SHIA** na vyama vya watu wenye ulemavu Tanzania chini ya shirikisho la **SHIVYAWATA**

Shukrani za dhati kwa wote walioshiriki katika kufanikisha uchapishaji wa kitabu hiki.